# Blogger somo la 1: Jinsi ya kutengeneza Blog

Somo hili litakwenda kukufundisha hatuwa kwa hatuwa jinsi ya kufunguwa blog kwenye mtandao wa blogger.

JINSI YA KUTENGENEZA BLOG KWA KUTUMIA BLOGGER:

Post hii inakwenda kukufundisha jinsi ya kutengeneza blog yako mwenyewe kwa kutumia mtandao wa blogger. Haya ni maelekezo mafupi ambayo yanatumia dakika zisizozidi 10 mpaka kukamilisha kuwa na blog yako.


Vigezo:

1. Uwe na email ya **gmail**
2. Uwe na simu ama kompyuta
3. Juwe kusoma na kuandika

Kama upo tayari kuanza kufunguwa blog yako. Fuata maelekezo yafuatayo.


1. Kingia kwenye tovuti hii [blogger.com](blogger.com)

Kama huja log in upande wa kulia wa ukurasa huu kwa juu kuna sehemu imeandikwa **sign in** utabofya hapo ili kulogin kwa email ya gmail. Kwa juu katikati chuka chini kidogo kuna batani imeandikwa **create your blog** bofya hapo. Angalia picha hapo chini. Kama hujalogin utaendelea ku login ama kama tayai utapelekwa ukurasa mwingine.





1. Baada ya hapo ukurasa utakaofunguka utakuhitaji kuweka jina la blog kwenye **Title** jina lisizidi herufi 100. Ni vyema jina likawa fupi na lenye kueleweka vyema. Kwa mfgano tutakwenda kutengeneza blog yetu yenye jina la tehama. Hivyo kwenye Title nitaweka

**Tehama**. Kisha baada ya kuandika jina la blog utabofya **next** chini upande wa kushoto. Angalia picha hapo chini.





Baada ya hapo ukurasa mwingine utafunguka. Huo utakuhitaji kuweka anuani ya blog yaani **address** ama **url**. Hii ni link ambayo blog yako itapatikana. Hapo utajaribu maneno kadhaa ambayo yanaendana na jina la blog yako. Kama hamuna blog ambayo ina url sawa na hiyo unayoweka itakubaliwa, ila kama imeshatumika itakataliwa.




Anjani yako ifuate sheria hizi:-


1. Usiache nafasi kati ya neno na neno
2. Usitumie special character kama @, %, #, na nyinginezo kama mabano
3. Vyema usitumie namba tupu ambasuchanganye namba na herufi
4. Vyema isiwe ndefu
5. Usichanganye herufi ndogo na luwa
6. Anuani iwe rahisi na yenye kueleweka.

Kama nilivyokueleza awaku, hapo unaweza kuweka maneno kadhaa yakakataliwa. Wacha tuweke tehama uone kama litakubaliwa.





Utaona hapo tumeambiwa **address is not available** yaani hiyo anuani tayari imeshatumiwa. Hivyo tutajaribu ningine. Utaona hapo mbele kuna neno **blogspot.com** hii ni domain ambapo blog yako itakaa. Utakapotaka kuondosha hayo mabneno utatakiw akununua jina yaani domain. Nitakufynsiha mbeleni.

Sasa nakwenda kuweka neno **tehamatzbongo.** Utaona hapo chenye picha nimembiwa **this address is available** maana yake anuani hii ipo. Hivyo blog yetu itaipatikana kwa link hii **tehamatzbongo.blogspot.com** kwa wewe u=utatafuta neno ambalo litakuwa tayari. Baada ya hapo utabofya **next** kwa chini upande wa kushoto.




Ukurasa utakaofuata utakuhitaji kuweka jina ambalo litakuwa likionekana kwenye blog yako. Unaweza kuweka jina lolote ila lisizidi herufi 200. Hapa sitokwenda mbali sana na jina tuliloweka mwanzo. Hapa nakwend akueka **Mafunzo ya Tehama.** Baada ya hapo bofya neno **finish** kwa chini upande wa kulia.




Mpaka kufikia hapo blog yetu imekamolika. Kutaka kuiona blog yetu bofya hapo palipoandikwa **view blog** chini kapisha nimeweka namba 2 . Utaona kajiblog ketu hapo tayari. Ila sasa haina post hata moja. Somo linalofuata litakwenda kukufundisha jinsi ya kuandika post. Blog yetu tulioitengeneza utaipata hapa https://tehamatzbongo.blogspot.com/

**Mwisho:**

Katika somo linalofuata utakwenda kujifunza jinsi ya kuandika post yako ya kwanza. Ama unaweza

kufanyia mazoezi hapo nilipoweka nmaba 1 kwenye picha hapo juu.


...**Makala hii imeandaliwa na Bongoclass. Kupata makala zaidi, tembelea website yetu: www.bongoclass.com**

**Kitabu hiki kina muendelezo kwa ajili ya mafunzo zaidi. wasiliana nasi kupata kitabu kizima**...

# BLOGGER somo la 2: Jinsi ya kuandika post na kuiboresha pamoja na kuidhibiti


Katika post hii utakwend akujifunza jinsi ya kuandika post, kuisimamia na kuoboresha.

Kama unatumia simu upande wa kushoto kuna menu hapo bofya utaletewa list ya menu. Bofya palipoandikwa **NEW POST**. na kama unatumia kompyuta bofya palipoandikwa **NEW POST** upande wa kushoto kwa juu.





Kama unatumia simu ukurasa utakaofunguka utakuwa tofauti na wanaotumia kompyuta. Hata hivyo nitafafanua kwa manufaa ya wote wanaotumia simu na kompyuta. Hapo chini naleta picha mbili moja kwa wanotumia simu na ingine ni kwa wanaotumia kompyuta.

**Kwa watumiaji simu**





**Kwa watumiaji kompyuta**




1. Hapo kwenye namba 1 ndipo utakwenda kuandika kichwa cha habari cha hiyo post yako.
2. Kwenye namba 2 ni kwa ajili ya ku preview yaa ni kuangalia jinsi ambavyo post yako itaonekana na wasomaji wako kabla hujaipost
3. Kwenye namba 3 hapo ndipo utakapobofya pindi unapomaliza. Ukibofya hapo post yako inakuwa live. Hivyo watu wote wataweza kuiona.
4. Hiyo ni menu ambapo kila unachokiona hapo kitakusaidia katika kuboresha muonekano wa post. Kwa wanaotumia siku buruza huo mstari utakuonyesha menu zaidi.
5. Kwenye nmaba 4 hapo hutumika ku edit html code za hiyo post yako. Kama unataka kuongeza maboresho kwa kuweka code za html, css na javascript kwenye post yako, basi hapo ndio sehemu inayotumika.

**Menu ya vifaa vya uandishi**

Sasa ngoja tuone baadhi ya sehemu muhimu katika uandishi wa post yako kwenye blog.




1. Ni kwa ajii ya kufanya herufi kuwa bold
2. Ni kwa ajili ya kufanya maandishi kuwa italics
3. Ni kwa ajili ya kupigia mstari maandishi
4. Kwa ajili ya kukata maadhishi
5. Kwa ajili ya kuweka rangi kwenye maandishi
6. Kwa ajili ya kuweka rangi ya background
7. Kwa ajili ya kuweka link
8. Kwa jili ya kuweka picha
9. Kwa ajili ya kuweka video na audio
10. Kwa ajili ya kuweka emoj
11. Kwa ajili ya kupangilia muonekano wa paragraph
12. Kwa ajili ya kupangilia mtiririko wa namba
13. Kwa ajili ya kunukuu

**Mfano wa post**

**Ni nini maana ya blog**



Neno **"blog"** linatokana na neno la Kiingereza "weblog," ambalo ni kifupi cha maneno "web" na "*log*." Katika Kiswahili, "blog" inaweza kutafsiriwa kama "blogu."

Blogu ni aina ya tovuti au ukurasa wa mtandao ambapo mtu au kikundi cha watu hutoa maudhui yanayopangwa kwa utaratibu wa wakati, na mara nyingi maudhui hayo yanahusu mambo ya kibinafsi, uzoefu, maarifa, au mada nyingine zinazovutia mwandishi wa blogu au wasomaji wake.


Mwandishi wa blogu hujulikana kama "blogger," na anaweza kuchapisha machapisho (posts)

mapya mara kwa mara. Hii inaweza kujumuisha maandishi, picha, video, au hata sauti. Watu hupenda kufanya blogu kama njia ya kushiriki uzoefu wao, mawazo, au maarifa na wengine kwenye mtandao.

Blogu zinaweza kuwa za aina nyingi, kama vile blogu za kibinafsi, blogu za habari, blogu za mada maalum, na kadhalika. Ni jukwaa lenye mwingiliano na huruhusu watu kutoa maoni na kushirikiana na mwandishi na wasomaji wengine.

Weka post hiyo ukimaliza weka na picha, baada ya hapo bofya batani ya ku publish rejea picha hapo juu namba 3. Ukisha bofya utarudishwa kwenye dashboard. Dashboard hiyo itakuletea vitu vingine vipya.

**Kwa watumiaji wa simu:**




**Kwa watumiaji wa kompyuta:**

1. Hiyo ndio menu ambapo watumiaji wa simu atabofya ili kupata menu kuu
2. Hapo panaonesha tarehe ambayo post iliandikwa. Pia kwa watumiaji wa kompyuta ukiweka cursor hapo ndpo utapata menu kuu hiyo. Kazi nyingine ya hapo ni kuwa ukibofya utakwenda ku edit post. Hivyo kama unataka kuifanyia mabadiliko bofya hapo
3. Ni kwa ajili ya kufuta post.

4. Kwa ajili ya kuweka lebel
5. Kama hutaki post iwe live kwenye blog utabofya hapo, post itakuwa ni draft
6. Hiyo ni kwa ajili ya kuangalia post yako live.

Pia kuna menu nyingine ndogo chini ha hiyo menu kuu, angalia picha hapo chini:



1. Hiyo ni kwa ajili ya ku share post yako
2. Hiyo inaonyesha idadi ya comment kwenye hiyo post
3. Hiyo ni kuangalia comment
4. Inaonyesha idadi ya watu walioisoma
5. Ni kwa ajili ya kuagalia takwimu zinazohusu hiyo post

Mwisho:

Tukutane somo linalofuata tutakwend akujifunza jinsi ya kuifanya blog yako ionekane Google.

...**Makala hii imeandaliwa na Bongoclass. Kupata makala zaidi, tembelea website yetu: www.bongoclass.com**

**Kitabu hiki kina muendelezo kwa ajili ya mafunzo zaidi. wasiliana nasi kupata kitabu kizima**...

# BLOGGER somo la 3: Jinsi ya kuifanya Blog yako iweze kuonekana Google kwa urahisi

Katika somo hili utakwenda kujifunza jinsi ya kuifanya blog yako iweze kuoneka Google kwa urahisi

**JINSI YA KUIFANYA BLOG IPATIKANE KWENYE SEARCH ENGINE KAMA GOOGLE**

Search engine (Injini ya utafutaji ni nini?

Injini ya utaftaji ni mfumo wa programu ambao umeundwa kutekeleza utaftaji wa wavuti. Wanatafuta Wavuti Ulimwenguni kote kwa njia ya kimfumo kwa habari fulani iliyobainishwa katika swali la utaftaji wa maandishi. [Wikipedia (Kiswahili)]

Ni kazi yake Search engine yeyote iwe google ama nyingineyo kutafuta web ama blog yako popote ilipo. Ama kutafuta post ulioiandika popote pale ilipo. Hata hivyo hutokea kuwa ikashindwa kuona hiyo blog yako ama post yako. Hivyo utahitajika kuisaidia kujuwa namna ya kupata blog hiyo ama post yako. Zifuatazo ni njia za kuifanya blog yako ionekane kwenye search engine:-

1. Ruhusu blog yako ionekane kwenye search engine. Kwa wale wanaotumia blogger kuna mambo kadhaa unatakiwa uyafanye kwenye setting. Mambo hayo ni kama:-


    1. Ingi kwenye setting utaiona kwenye menu upande wa kushoto kisha kwenye kipengele cha Privacy kuna palipoandikwa ***Allow search engine to find your blog*** washa hicho kibatani.
    2. Kwenye hiyo setting shuka shini kuna palipoandikwa ***Crawler and indexing*** washa hicho kibatani kilichoandikwa ***Enable custom Robot.txt***





Kwa wale ambao wanatumia wordpress ama website zao huna haja ya kufanya jambo lolote zaidi ya kusubiri hatuwa inayofuata. Kwa sasa hakikisha kuwa blog au website yako haihitaji password ili kuweza kuifikia. Ama kurasa ambazo unahitaji zionekane kwenye search engine hazihitaji mtu kulogin.

2. Isajili blog ama web yako kwenye search engine. Karibia search engine zote kubwa zina mfumo wa kuisajili website ama blog yako. Kwa mfano kwa google wanatumia [Google Search Console] kwa microsoft bing wanatumia [Bing Webmaster Tools] kwa yandex wanatumia [Yandex Webmaster] na zaidi ya hapo. Katika somo hili tutakwenda kuitumia **google search console.**


Unachotakiwa kufanya ni kujisajili kwenye hizo search engine kwa mfano Google search console [Kwa kubofya link hii https://search.google.com/search-console]. Utalog in kwa email yako, kisha Utatakiwa kuweka link au domain ya blog au website yako. Kule itaitwa property.





Kama hujanunua domain, weka link ya blog yako hapo palipoandika URL prefix. Kopi vyema link ya blog yako . Link utaipata kwenye upau wa juu wa kivinjari chako cha intanent. Angalia picha hii





Baada ya hapo, Pest hiyo link kwenye hicho kibox kilichoandika URL prefix. Itaonekana kama kwenye picha hapo chini




Hatuwa inayofauata bofya hapo palipoandikwa continue, itahitaji kufanya verification. Kwa wale wa blogger itajiverify yenyewe. Kama unatumia blog iliyo tofauti na blogger watakupa njia nyingine za kufanya verificationa kama kwa kutumia DNS kwenye domain, ama utapewa html code uziweke kwenye <head> ya blog ama website yako.





Pindi verifikation ikawa tayari bofya hapo palipoandika GO TO PROPERTY. Hpo moja kwa moja utapelekwa kwenye dashboard. Hapo utakuwa umeshaisajili web au blog yako kwenye search console ya google. Hivyo basi bofya START kuanza.




Kuna mambo mengi sana utatakiwa kuyajuwa hapo baadaye. Kwa sasa nitakueleza hili. Tunatakiwa tuongeze site map. Na utafanya hivi kila baada ya masiku kadhaa. Ijapokuw ahili sio la lazima kwani google wenyewe wanaitafuta blog iliyopo kwenye blogger. Lakini utahitajika kufanya hivi mara kwa mara kama unatumia website hasa zile za html.


Kwenye dashoard kuna palipoandika SITEMAPS. Kikawaida search engine huhitaji sitemap ili kuweza kuziona post au makala zote zilizomo kwenye blog ama tovuti husika. Kwa wale wa blogger utainia hapo site map kisha




Kisha kitakuja kijibox ambapo utatakiwa kuweka link ya sitemap. Wale wa blogger hapo weka sitemap.xml kama inavyoonekana kweye picha hapo chini. Na wale wanaotumia website za html, au wordpress ama blog nyinginezo utahitajikakutengeneza sitemap yako kisha unakuja ku pest link hapo.





Kutengeneza sitemap utahitajika kufuata maelekezo vyema ama tumia website hii [http://www.check-domains.com/sitemap/index.php](http://www.check-domains.com/sitemap/index.php) hapo utatengeneza site map, kisha uta iupload kwenye web yako. Kisha utachukuw alink na kuja kuipest hapo. Ukimaliza bofya submit. Kama imekubaliwa utapokea ujumbe huu




Vinginevyo utarudia. Lamda tu nikujuze kuwa sitemap inakuwa na orodha ya post zote, au makala

zote. Hivyo maroboti ya search engine watatumia hiyo kama kielekezi cha kuangalia post ambayo haipo kule ama imefanyiwa marekebisho na kuiupdate kwenye search engine.




Kila utakapoona kuna post au makala mpya na haipatikani kwenye search engine ni vyema utengeneze site mapa ambayo itakuwa na link ya hiyo post au makala mpya.

Mpaka kufikia hapa utakuwa umesha ifanya blog ama web yako ipatikane kwenye Google search engine.

3. Shea blog ama web yako zaidi na zaidi.

Kama nilivyokueleza kuwa search engine zitaitafuta web/blog yako popote pale ilipo. Hivyo kila ukishea ndipo unawarahisishia hawa maroboti quinoa hiyo post au maka. Unaweza kutumia facebook, youtube comment box, blog comment box na social media nyingine.

4. Hakikisha blog ama web yako ni salama. Search engine wataikataa link yeyote ile ambayo haipo salama. Na wanaweza pia kuifunga web ama blog yako.

5. Andika maudhui nzuri, wacha kukopi na kupest mitandaoni. Tumia lugjha nzuri. Pia hakikisha hiyo blog ama tovuti ni rahisi kuitumia. Pia kurasa zote unazotaka zionekane kwenye search engine hazihitaji kujisajili.

**Mwisho:**

Kwatika somo linalofuata tutakwenda kujifunza jinsi ya kubadilisha template ya blog ili kuboresha muonekano

...**Makala hii imeandaliwa na Bongoclass. Kupata makala zaidi, tembelea website yetu:**

**www.bongoclass.com**

**Kitabu hiki kina muendelezo kwa ajili ya mafunzo zaidi. wasiliana nasi kupata kitabu kizima**...